Com. Mosonik: Ameng'ang'ana na hiyo kazi sio rahisi. Kulikuwa na mzee mmoja anaitwa Mr Anthony Lusik wa Kipkelion Education Foundation. Alikuwa amejaribu kutafsiri maswala na maswali, issues and questions kwa lugha yetu. Sijui kama mlitumia wakati wa raia and then -----(inaudible) ng'alek che tinyegei ak Katiba ak tebutik che tot kotebengei commisionaek in Kalenjin na pengine mlifikiria kujadiliana, pengine itasaidia. Kama basic rights Imanit ab chito kama hii aliita mazingira , aliita ole wu emet ak makarnatet ab indet from the beginning. So unaweza kuitumia kwa ajili hizi lugha zimekuwa ni ngumu na asante sana kwa kujaribu.

Sasa mwenzangu Mary ametaja ukurasa la kumi na nane chapter 18, hiyo inaitwa, the Amendment of the Constitution ama kwa Kiswahili kubadilisha Katiba na mwenendo au utaratibu wa kubadilisha Katiba. Ningependa kuisitiza kwamba hilo swala ni muhimu kwa vile nyinyi wote mmeshugulikia maneno ya kurekebisha Katiba, kubadilisha Katiba hii. Kuunda upya, kugeuza Katiba halafu pengine kesho mtu aje aubadilishe siku moja, hii kazi yenu yote mlikuwa mnafanya ilikuwa ni ya nini. Kwa hivyo nitawauliza kusoma ndiyo muelewe zaidi uwakumbushe kwamba Katiba ya Kenya imeenda stages tuseme mbili.

Wakati wa uhuru kulikuwana Katiba ya uhuru inaitwa independence constitution ambayo iliandikwa Lancaster House, Kiingereza na viongozi vya vyama vya kiasi. Nakumbuka kwanza kwamba kulikuwa na viongozi watu kumi na wanne halafu

mwishowe wakaongezeka wakawa watu thelathini na tatu. Wa kwanza walikuwa akina Musinde Muliro, Tom Mboya, Oginga Odinga, Samuel Ayodo, Ole Tipis, Robert Matano, Ronald Ngala, Jeremiah Nyaga, Gikonyo Kiano, Mate, Arap Moi, Arap Towet na kadhalika. Wale ambao waliandika Katiba wakandika kuanzia mwaka wa 1963 mpaka mwaka wa sitini na tau. Tulipopokea uhuru mkiangalia kwa TV ile sherehe ya kwanza ya uhuru wa mwaka wa 1963 tarehe kumi na mbili mwezi wa December.

Hiyo Katiba Mzee Kenyatta akiwa Waziri Mkuu alikuwa anapokea instrument of power na moja za hizo, zilikuwa ni Katiba na tena coming into operation before 12th December 1963 Katiba hiyo ilikuwa ni hii. Ilikuwa Katiba ya ukurasa, chapter ni hii inaitwa sura. Sasa hii ilikuwa ukurasa mia mbili tisaini na tisa, 299 karibu tuseme mia tatu. Lakini tangu wakati huo Katiba hii ikafanyiwa marekebisho, ikabadilishwa. Ndiyo tunasema sasa kwa miaka hii thelathini na tisa ya uhuru imebadilishwa karibu mara thelathini na tisa.

On average inabadilishwa mara moja kila moja mapaka Katiba hii ya uhuru imekuwa hii sasa. Wakati wa elimu ya uraia watu wengi hawajaiona Katiba ya Kenya. Ile tunarekebisha ni hii wakati wa uhuru ilikuwa ni hii. Ikabadilishwa mpaka sasa ukiangalia hii ni ukurasa 98 pages. Original ilikuwa 299 pages. Tuseme kwa hii miaka thelathini na tisa page mia mbili ikafutuliwa mbali. Ikabadilishwa na ikabadilishwa na nani? Na Wabunge. Iliandikwa na viongozi wa siasa. Wengi wao wote walikuwa ni wanaume wale wazee walienda Lancaster. Walikuwa wanaume ijapo mama moja tu alitoka North Nyanza, Western Province alitwa Priscila Apiyo not Asiyo Abwao. Lakini tulikuta huyo mama akatueleza tulipokuwa Lancaster kazi yangu ilikuwa na kuwapikia hawa wanaume ndiyo wapate nguvu ya kuunda Katiba.

Tuseme kwa hivyo iliandikwa na viongozi wa siasa wa wa Afrika na wengine na ikabadilishwa na wa Bunge. Lakini hii Katiba ya kwanza ilikuwa na utaratibu wa kubadilishwa na haikuwa ni rahisi sana vile ilikuwa imeandikwa kuibadilisha. Kulikuwa na sehemu zinaitwa entrenched clauses. Hizo ni sehemu ambayo ilikuwa ni huwezi kubadilisha ama ukibadilisha na ngumu sana na sehemu zingine. Lakini hasa utaratibu ya kubadilisha hii Katiba ilibadilishwa. Kwa mfano, tunakumbuka tulikuwa na Senate na Lower House na kubadilisha wanweza kupendekeza Lower House lakini lazima iwe approved by the Senate. Kwa hivyo kuulikuwa kuna stage ya badilisho lakini ndiyo ikang'olewa ndiyoikawa rahisi sana ibadilishwe.

Sasa kwa hivyo msome sura ya kumi na nane ukurasa wa thelathini na sita. Page 36 chapter 18 na inasema amendment of the Constitution. Inasema kwamba sasa kwa ajili kutakuwa na nyumba mbili ya Bunge, kuibadilisha lazima ikubaliwe na nyumba hizo mbili za Bunge lakini hizo nyumba mbili sio zile za wakati wauhuru. Wakatu wa uhuru zilikuwa zinaitwa Senate na House of Representatives or Lower House. Sasa kutakuwa na National Assembly na National Council. Mtaelewa tofauti lakini kuna procedure kwamba mswada ikipendekeza kwa nyumba moja lazima hata ile ingine ikubali. Kitu cha kwanza lakini ukitaka kubadilisha territorial ya Kenya mpaka ya Kenya au utawala ya wananchi, the sovereignty of the people au yale malengo ya taifa, madili na kanuni. Ile Arap Rotich aliita *ole lite emet* yaani direction ya nchi. *Nga'tutik che mwaie ole lite emet.*

Ukitaka kubadilisha hiyo au ile sura kuhusu sheria ya haki, bill of rights, *Imanit ab chito* au ile serikali inasemekana inaletwa karibu na raia hiyo structure of devolution au kuhusu uraia wa Kenya au chapter hii yenyewe, lazima wananchi wakubali hii. Entrenched clauses katika hii Katiba ndiyo hiyo. Yawe ni mambo makuu kabisa. Mtaangalia na kusema je! Na hizo pekee zao? Tunataka raia waulize maoni yao ama tuonge sehemu nyingine ama tupunguze. The procedure for amending the Constitution.

Ikiwa nimesema hivyo, tafadhali sasa tuangalie ukarasa wa thelathini na saba. Inaitwa schedules katikati ya ukurasa. Schedules kwa Kiswahili zinaitwa nyongesa. Hizi ni nyongesa kwa Katiba. Nyongesa ya kwanza inaitwa territory of the republic of Kenya na hiyo ni kusema amepaka vile tumeelezwa na mwenzangu hapa. Hiyoni kusema mipaka vile tumeelezwana mwenzangu hapa. Hii ni mara ya kwanza, territory ya jamhuri ya Kenya imeandikwa kwa Katiba. Katiba hii ya sasa inasema Kenya ni jamhuri inayojitawala lakini ukiuliza mipaka nio wapi? Hakuna. Ndiyo pengine wale ma shiftar walikuwa wanasema North Eastern kidogo ni yao. Watu wengine bandits wamekuwa wakitoka Ethiopia wanasema area ya Moyale hata ni yao. Iddi Amin mwaka wa sabini na mbili akasema mipaka ya Kenya na Uganda ikoNaivasha mpaka tukafanya mandamano.

Wakati huu tunasikia kwamba kwa lake Victoria majeshi ya Uganda wanafukuza raia wetu wakifanya mambo ya kiuchumi. Page 37 mpaka 412 ni mipaka. Inasema mipaka ya Kenya –Uganda, Kenya-Sudan, Kenya –Ethiopia na bahari sehemu za bahari ya Kenya. Kenya –Tanzania naimeonyesha beacons ukiangalia hivyo iko beacons. Kwa ile Katiba ya kwanza ya mwaka wa sitini na tatu kulikuwa na mipaka imeandikwa kwa beacons wakati huo na leo nitajaribu kupata Kericho district. Wakati ule yaani mipaka ya district imeandikwa kwa beacons, Narok district, Kericho district.

Page 261 ya Katiba ya mwaka 1963 ilisema the Kericho district moja ya wilaya arobaine na moja wakati ile. Kuazia trigonometrical point Kelegele in the South West corner of original na hiyo shamba iko LR No. so and so, generally Manga Hills reach, halafu inaenda kufuata Kisii- Sotik road reserve. Halafu Eastern boundary of Kericho –Sotik road reserve. Halafu two rivers which are not named South of Kipsonoi Hill ilikuwa na mipaka lakini mipaka ya district . Sasa hii ina mipaka ya Kenya mwenyewe, schedule number one. Number two page 41, kuna orodha ya mikoa ya Kenya ambayo ni nane halafu na districts chini ya hii kila mikoa. Tunasema Nairobi Province one district, Rift Valley kumi na nane na zote wilaya ni ukienda the next page, ukifanya hesabu ni sabini. Ni muhimu kujua hiyo kwamba ni sabini zimetajwa lakini beacons hakuna. Lakini kwa Katiba ya kwanza ilikuwa ina beacons.

Haya ya tatu ni vile tumeelezwa national symbol, Bendera ya Kenya, Wimbo wa Taifa, Court of Arms.

Ukurasa wa arobaine na mbili mpaka arobaini na nne inasema kuhusu kiapo ya afis. Mtu akiwa atakuwa Rais ama Wakamu wake ama Waziri Mkuu au Waziri au Naibu wa waziri ama Permanent Secretary au Judge ama Commissioner au kiongozi wa mkoa ama district na Speaker na kadhalika. Halafu page 44 sasa tuangalie hapo hiyo inaitwa nyongesa number five. Inaitwa leadership and Integrity code of conduct. Yule rafiki yetu anaitwa “*atepto ne mie en kandoinatet*” sasa hiyo pengine tuangalie kwa makini. Yaani inapendekezwa kwa Katiba mpya kwamba viongozi watakuwa na tanuni waongozi na watakuwa wanatakiwa wafuate. Kwa mfano, watakuwa wanasema mfanyikazi wawe wa uma hawezi kupokea mishahara mbili yaani

kufanya kazi mbili na kupokea mishahara.

Kitu cha pili kiongozi ameruhusiwa kufany biashara ama kulima. Nakumbuka Ndegwa Commission ndiyo aliwaruhusu civil servants toengage in his business. Hii tunapendekeza waendeleee kufanyha biashara au ukulima. Kitu ingine Rais, Makamu, Waziri mkuu, Mawaziri, zote na wakubwa, naibu wake watatakiwa na viongozi wengine kutangaza mali yao. Inaitwa declaration of assets and liability. Na mtu ambaye amechaguliwa kuwa Rais ama Wakamu wake kabla kuanza kazi yake ni lazima atangaze mali yake na hiyo mali akitangaza kuna register fulani inafunguliwa na inaandikwa hapa. Kama wakisema uongo na ipatikane wamesema uongo hiyo ni kosa na anweza kuhukumiwa kortini.

Na kila mwaka, lazima atangaze tena. Mwaka huu aseme zilikuwa hivi ikiongezeka atangaze tena na kusema imeongezeka vipi kwanjia gani? Kuna maadithi ya kufanya kazi kwa ma ofisi za uma. Watu wakija kisiasa lazima mjue kwamba wewe ni mfanyi kazi wao sio boss wao wakiadhuru wananchi, kina mama wanaokuja kutafuta usaidizi kwa ofisi ya serikali na unamsumbua.

Kitu kingine ni kwamba kama kiongozi unafanya kazi unaenda kazi ya serikali halafu wananchi wanafurahia unapatiwa zawadi ya kushukuru. Hiyo zawadi si yako ni ya ofisi kwa ajili hukuwa unaenda kibinafsi kufanya hiyo kazi. Kwa hivyo, kama ni mbuzi unapeleka mpaka ofis na kuacha kwa ofisi na mambo kadha wa kadha. Kwa hivyo ninawasihi nyiyi wote msome kwa makini pages 44, 45, leadership integrity, code of conduct. Kama mnakubaliana au kaipunguzwe na whom should it apply to. okay. It is very important and it is intended to curb corruption this particular schedule. Page 45 schedule number sita.

Actions to be taken by Parliament. Hapa inaonekana kutakuwa na mabadiliko mengi. Je! yatatekelezwa nini kulingana na Katiba mpya na mpangilio la tume la marekebisho ya Katiba. Inginge inasema six months, ingine inasema one year, ingine two years na ingine three years. Inginge inasema no time limits lakini ile imeandikwa time limits ninapendekezo kwamba itekelezwe kwa miaka mitatu. Kwa vile mnaweza kujuliza hii maneno yote itafanyika lini? Mabadilio haya yote tukikubali hii Katiba imeonyeshwa kwa hii program of action of implementation.

Page 46 kuna nyongesa namba seven na ikiwa muangalie kwa makini. Hiyo inaitwa powers of National and District Governance. Najua kwamba vile mwenzangu amependekeza kuna pendekezo utawala uje ukaribie ya ajabu na tunasema na mnaelezwa kwamba main focus ya powers kutakuwa kwa Province, kwa village ama location lakini main focus ni district. Manaelewa. Sasa hapana orodha ya kazi na uwezo wa serikali ya Nairobi tuseme list number one. National Government list , kazi ya serikali kuu kutakuwa ni fulani. Halafu list namba two ni ya serikali ya wilaya, district government list. Katikati ya ukurasa kuna list number three concurrent list kazi ya sambamba ya serikali kuu na serikali ya wilaya. Mjue responsibilities kwa ajili pengine kama utawala unakuuja kwetu kwa district tunapenda sana utawala lakini mkielezwa ufanye hiyo kazi kwa district hautaweza.

Kwa hivyo, mchunguzee kwa makini nimesema nini? What is the responsibility of the district government?

- a) Kwa mfano number two Local services will be used there for educational services, nursery, primary and secondary education.
- b) Medical and health services, health centers, dispensaries, clinics, promotion of primary health care.
- c) Water services
- d) Road services, construction, rehabilitation and maintenance and so on.

Sasa district itaweza kufanya hii au la? Na central government imepewa kazi za kutosha kama hizi kupunguzwa ama kuongezwa, chungu zenu vizuri. Wakati wa uhuru serikali ilikuwa karibu na raia hata wakati ule na kulikuwa na list kama hii lakini focus ya utawala wa wakati ule haikuwa ni district ilikuwa ni the wazee walikuwa 64, ilikuwa ni majimbo. Hiyo ni kweli? Majimbo ilikuwa ni nini Province? Province wakati wa ukoloni ilikuwa inaitwa Provinces, Mikoa. Tulipopata uhuru ikaitwa regions na kulikuwa na regions na kulikiwa na orodha za regions za Kenya. Iisema Kenya should be divided into Nairobi area in the following regions: Coast region, Eastern region, Central region, Rift Valley region, Nyanza region, Western region and North Eastern region halafu kila region ilikuwa imetajwa district chini yake. Sasa utawala ilikuwa kwa majimbo. Kulikuwa na mapendekezo kuhusu majimbo wakati tulikusanya maoni.

Nimesoma gazeti ya leo, East African Standard, Thursday October 17th. Hata hiyo swala iliulizwa Nyeri kwa Commissioner ambaye alikuwa anafanya hii kazi jana. He said the Commissioner of Kenya Review Commission has admitted that views from certain parts of the country were omitted were left from the final draft because they were too sensitive.

Commissioner Dr Githu Muigai, told a section in Nyeri that views expressed in some communities would have polarized the divide Kenyans unless they were toned down. He gave the example of over views that Kenyans should adopt majimbo as proposed by several Province which was totally rejected in Central Province. He also said sentiments there were other things that were omitted because of controversy lakini kitu cha muhimu ni responsibility ya district government itakuwa ni what? Na ya Central government itakuwa ni what? Kwa vile unaweza kuwa na utawala lakini at the same time utaweza kuwa na shida kwa ajili ukieleza sasa barabara zote is your responsibility na pengine pesa hakuna. Please study this seven schedule.

Sasa eight schedule in page 46 inaitwa transitional and consequential positions. Number one ni Rais duties and obligations of the republic. Ukiwa na Katiba mpya every thing that was responsibility ya jamhuri ya Kenya itatekeleza kimataifa hatuwezi kubadilisha.

Number two inaitwa existing laws, ikiwa tumebadilisha Katiba na hiyo kuna sheria kanuni ya sheria Kenya ambazo ziko sasa je! nini itafanyika? Katiba ni sheria kuu kwa hivyo sheria zote zingine ambazo haziambatani na Katiba mpya zitabadilishwa.

Ya tatu ni kuhusu uchaguzi. Inasema ni lini uchaguzi ufanywe chini ya Katiba mpya kama hii Katiba itakuwa imepita? Haya number three.

Number four inasema tusome right hand corner please. Inasema at the top of page 46, a person who before the entry into the office of this constitution has held office for two or more terms as President is not eligible to:

a) Stand for elections or serve as President, Vice President, Prime Minister or Deputy Prime Minister, Minister, Deputy Minister, or Member of Parliament. Tunasema kwa ufupi yeyote ambaye amewai kuwa Rais kabla ya hii Katiba mara mbili hataruhusiwa kusimama, kuomba kura ama kufanya kazi kama Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Naibu wa Waziri Mkuu, Waziri Waziri usaidizi ama hatakuwa MP. Mnaelewa hiyo?

Number five inasema any person, who would otherwise been qualified to stand for election for the Commission of this constitution is eligible to stand for the candidate in the first election and under this constitution. Tumetoa qualifications of the President in the chapter four executive. Msome qualifications of the President ni gani lazima awe mtu wa high moral integrity. Lazima awe mtu wa miaka kati ya thelathini na tano na sabini na lazima awe na degree from a recognized university na kadhalika. Okay. Lakini tumesema wakati huu kama kuna mtu yeyote ambaye haitosheleshi hayo mahitaji, pengine kwa mfano hajapata degree ya university ama pengine yuko chini ya miaka thelathini na tano ama amefikisha kidogo sabini tutaruhusu kusimama kwa uchaguzi ujao mnaelewa? Hiyo inaitwa transitional clauses.

Bottom of page 46, naona imeandikwa Provincial Administration. On the coming unity of force of this constitution the system of administration comprising Chief, Sub-Chiefs, DO's, DC's and PC's on the following page commonly known as Provincial Administration shall turn dissolved. Kwa Kiswahili inasema wakati wa kutekeleza Katiba hii jukumu la utawala unaoitwa utawala wa mkoa utatupiliwa mbali. Secondly it says na wale watuwaliokuwa wakifanya hiyo kazi ni nini itafanyika? They will report to the Public Service Commission for re-deployment kuna existing offices.

Kuna maneno ya Judiciary, mahakama na mmesikia kumekuwa na kesi kortini. Hata hatujui kusema tutasema ndiyo tumeweka hizi zote. Mnajua hiyo shida? Lakini tumetengeza hata isipopitisha hii kuna mambo yatafanyika kuhusu courts na Judges. Middle of page 47 is death penalty and other outlawed services. Hukumu ya kifo mmeelezwa na rafiki yangu kwamba hukumu ya kifo itatupiliwa mbali. Nimependekeza kwamba mtu yeyote ambaye alihukumiwa kunyongwa under 1313 na amemaliza ile maneno ya kukata rufai. Anangoja tu kunyongwa. Sasa kunyongwa hakutatekelezwa na automatically everything will be reduced to life imprisonment. Itakuwa ni hukumu ya kufungwa maisha na tena wanaweza kuendelea wanaweza kusamehewa. Mnajua kuna kitu inaitwa remission for sentence na vitu kama hiyo lakini hukumu ya kifo should be stopped hata retrospective. Understand that.

Ya tatu, every sentence of corporal punishment passed before the coming into force of this constitution, is remitted and shall not be carried out. Ile maneno ya kusema kuwa mtu amehukumiwa kuchapwa kiboko kumi na mbili ama moja itakoma. Hawatapigwa wale wanapigwa----- (inaudible)

Haya Constitutional Commission, Interim Judicial Service Commission. Page 47 the last column inaitwa first human rights abuses and I think you want to lead us the Commission of human rights and its structure, shall within six months of the coming into force of this constitution on the petition of any person or on its own motion shall :

- a) investigate all form of human rights submitted by any person or group for the coming operation of this constitution.
- b) Investigate the causes of civil strife including massacres, tribal clashes and identify those responsible
- c) Make appropriate recommendations regarding prosecution of those responsible, award of compensation to victims, reconciliation and referations.

Kwa hivyo kutakuwa na tume hii ya haki ya kibinadamu na ikipitishwa Katiba kwa muda ya miezi sita itatakiwa kuchunguza maneno yale yote ya kiuka haki, utiukaji ya haki ya kibina damu za wakati ziliopita. Kuchunguza ni kwa ajili gani yalifanyika. Nani alianzisha na wale walianzisha wahukumiwe na wale walipoteza mali yao wapewe ridhaa na halafu kupatanisha wananchi ndiyo wasikizane.

Finally kuna something about ownership of land. Hiyo msome pamoja na ile ukurasa ama sura chapter eleven kuhusu land and property because it was explained policy framework for land. Nafikiri nimemaliza. Now yes very quickly please. Sasa tumeangalia kwa ufupi. Mtaenda kusoma nyinyi wenyewe. Msome tena mara mbili mara tatu lakini tofauti ya hii Katiba sasa tunapendekeza na ile Katiba ya sasa hii ni gani kwa ufupi? Mnajua tumesema kwa ufupi ukiangalia hii na ile ya kwanza mnaona tofauti. Moja ni kubwa na ingine ni ndogo sana. hatujachapa hii ndiyo tujue itakuwa kubwa zaidi ya hii ama ndogo lakini tukiangalia ni sura ngapi iko. Hii ilikuwa sura kumi na nne, hii ingine sura kumi na mmoja. Hii tumeangalia saa hii ni sura ishirini. This one is eleven chapter that means there is more in the new Katiba than the old one. Mfanye kujua what is more in the new Katiba lakini kitu kimoja ni kwamba procedure, vile tuliandika hii Katiba ni tofauti. Hii iliandikwa na viongozi wa vyama wa siasa na ikabadilishwa na Wabunge. Hii tumehusisha wananchi tukiandika.

Haya kitu cha pili hatukuhuzisha tu wananchi tukiandika lakini tumeendelea kusema kuhusu wananchi kwa hii katiba. Chapter one, inasema sovereignty of the people. Uhuru ya wananchi na utukuu wa katiba. So people driven constitution versus the one ambayo it was Parliament driven.

Katiba hii tunapendekeza ina utangulizi, ina preamble, ina domain in the translation of the ----- (inaudible). Ile ya sasa haisemi chochote kuhusu utangulizi. Inaanza tu. One, Kenya is a sovereign republic, ina utangulizi. Wacha niende haraka haraka niwajulishe mambo mengine ambayo hata sijui wanajua. Kuhusu uraia Katiba iliruhusu kwamba mwana mume Mkenya akienda ng'ambo na akioa yule bibi wake wa ng'ambo akija na yeye Kenya bibi anakuwa automatic citizen na

watoto ni wa Kenya ingawa wamezaliwa ng'ambo.

Msichana wa Kenya akienda ng'ambo na apate mwanaume akaolewa. Yeye tunataka abaki ng'ambo na akija na huyo bwana yake wanaweza kukaa hapa Kenya na huyo mwanaume hapatiwi uraia na watoto wanangoja mpaka 18 ndiyo wa apply for Kenyan citizen. Kwa hivyo kwa ufupi kuna jaribio kwa hii Katiba mpya ya kuhuruzisha wanawake na wanaume, wasichana na wavulana, wazee na wamama.

In brief sasa tuseme kwa makini ile chapter tano sheria ya haki, the bill of rights, ndiyo muelewe kwa njia gani ama mbinu gani tumependekeza zitumiwe ndiyo kuzawazisha. That's okay the alance is here. Kitu kimoja tumeandika ni kuwa mwanamke na wanaume wana haki sawa lakini tumeendelea kusema kwamba kwa ajili sio sawa sasa, wanawake wapewe 30% of the seats in Parliament na mabo kama hayo.

Tumependekeza kwamba kuhusu kwa mfano watoto, tumesema watoto wote kama wamezaliwa ndani au nje ya ndoa wako sawa mbele ya sheria na wana haki sawa chini ya Katiba hii na hawa watoto wana haki na hata na jina. Outside of wedlock or inside. Tunasema mama yake na baba yake mtoto wawe wamefunga ndoa ama la wana majukumu sawa ya kulinda na kupatia mtoto mahitaji yake na kadhalika. Okay. I don't want to go in to details lakini *lakwet ab kap chi kesikchi lakwet ak itil kona*, haitawezekana kulingana na hii katiba. nisiendele sana lakini tumezawatisha rights kati ya men na women.

Kuna haki za mtu binafsi. *Imanit ab chito*. Tumeyaandika mengi mtayaona kwa hiyo chapter. Haki ya kuwa na elimu ya msingi mpaka ya secondary, basic education. Haki ya afya, elimu, nyumba, chakula, maji, mazingira na kadhalika. Lakini tumesema hizo haki serikali lazima itimize na tumepatia serikali itoe programe ya implementation of those rights. Kama hakuna pesa ni jukumu kwa serikali kuonyesha kwamba pesa kweli hakuna halafu ituonyeshe tena pesa itapatikana lini. Mnasikia? Ndiyo kutekeleza those rights.

Bunge itakuwa na nyumba mbili, National Council and National Assembly. At independence, ilikuwa Senate and Lower House. Wakati huu ni moja tu ya wajumbe mia mbili na kumi. Kwa jumla Bunge imepewa more powers kushinda hii ya sasa. Can you go into the details under Legislature? Then kuwachagua Wajumbe na wengine kuna taratibu mbili. Wakati huu kuchagua mtu inategemea tu uwingi, majority of people ama plurality of votes. Watu watano wakisisimama kutaka Bunge tunasema the first one ambaye ana uwingi wa kura lakini sasa tutakuwa na hiyo na tena tutakuwa na viti tisaini, the ninety seats of political parties. we shall talk about that two systems of political voting.

Mtu ambaye siye member wa chama chochote anaweza kusimama kuwa Rais ama Wakamu wa Rais na Wakamu wa Rais na Rais watakuwa wanasimama pamoja, ama awe MP na kadhalika. Independent candidate sio kama wale wa Mwau. Mwau anasema yeye ni independent lakini yeye ana chama cha wale ambayo hawana chama. Inaitwa Party of the

Independent candidate of Kenya. Si hiyo ni chama tena ? Lakini wakati huu mtu ambaye ni independent pekee yake kabisa anaweza kusimama na kuchaguliwa na kuna -----(inaudible).

Sasa vyama vya siasa vimeandikwa katika hii Katiba mpya. Kwa hii Katiba ya zamani hakuna vyama vya siasa. Tumejua kwamba imekuwa Registrar of Society ambaye wanaregister political party. Sasa there will be registrar of Electoral Commission lakini kuna masharti ya kuregister au ya kuderegister.

Kwa mfano chama cha siasa lazima ifuate kanuni cha kidemokrasia in its own internal affairs. Chama ambacho kitakuwa kina 5% ama zaidi ya kura zote itapewa pesa from political party fund kutumia in some ways. Kutakuwa na public fundings and political funds. MPs hawata tena amua maswala ya mishahara yao. Kutakuwa na Tume inaitwa Salaries and Remuneration Commission to decide salaries of the Mps. Tumeelezwa kwamba MP akipotelea Nairobi anaweza kuwa recalled. Sio lazima analize miaka mitano anaweza kurudishwa nyumbani na kuna procedure ya kufanya hivyo. Akiwa MP atassign hiyo leadership copy ambayo hakuna kwa Katiba ya zamani. Mjue kwamba tumesema kwamba MP hawezi kuwa Minister. Kwanza tunapendekeza ministries kumi na tano, wizara kumi na tano na wale wote ambao watakuwa waziri watatoka nje ya Bunge kama America. America Secretary of State Collins, Powell hakugania kiti cha Bunge. They are professionals. Tumesema kwamba watu wengi wantaka kuingi Bunge ndiyo walete bendera ipepee kwa constituency yao na akipewa bendera anaanza kuzunguka Kenya na kusahau nyumbani. Sasa tukasema they should not have a necessary burden wacha wakuwe tu MP kama American Congress.

President atakuwa na less power. Wengine wamesema ni ceremonial lakini hatujui lakini tumesema ni less powers. Mbinu ya kuchagua President imebadilishwa wakati huu ni 25% in all Provinces na wengi. Tumependekeza kwamba mtu akitakla kuwa President apate 50% ya kura zote na 20% in five Provinces. tulisema inaonekana hii 25% ni ngumu sana ndiyo tukapunguza iwe 20% lakini tumesema kama hakutapatikana mtu wa 50% na 20% kutakuwa na run off candidates number one na number two. Yule atashinda ndiye atakuwa na Rais.

Kutakuwa na Prime Minister ambaye atateuliwa na rais kutoka kwa kile chama chenye uwingi Bunge ama muungana wa vyama ambavyo wana win Bunge. President anaweza kuwa impeached. Hiyo hiko kwa Katiba ya sasa. Prime Minister anaweza kutolewa through a vote of no confidence. Kuna ile serikali ambao tulisema upunguzaji na utangazaji ya madaraka. Hii serikali ya devolved government. Ilikuwa kwa independent constitution lakini devolution ilikuwa Province. Ya hii ya sasa hakuna kitu kama hicho. Hii yetu tumesema iwe basically at the district level. Provincial Administration tumesema itupuliwe mbali. Provincial Administration haikuwa kwa hii Katiba lakini hii Katiba ilikuwa na kifungu na wacha nisomee nyinyi vile imesema.

Tulisema Provincial Administration kwa hii Katiba ilisema executive authority of the government of Kenya shall be in the President and subject to this constitution may be exercised by either directly or through officers, subordinates. Utawala ya

hiyo Provincial Administration tunaona imeandikwa office of the President. They were not there but they were created out of this constitution. Lakini sasa tumerecommend kwamba ufutuliwe mbali na hata kwa Katiba tumesisitiza avoidance of doubts. The present system and I'm almost through please just give me one minute so that you can understand.

Where is that can you please read it. On page 27, upande wa kushoto kabisa means staffing of devolved authority. It says for the avoidance of doubts, the system of Provincial Administration existing at the time of coming in to force of this constitution is abolished. So that is another difference between the two and then along side that administration police are to loose their separate identity. Administration Police imekuwa part of the Provincial Administration. So recommendation ni kwamba waingie kwa polisi ya kawaida. Kutakuwa na Supreme Court, kutakuwa na kadhi ile court ya kislamu imepewa nguvu zaidi kwa mambo ambayo yanahusu waislamu.

Polisi na kazi yao ya majeshi ya usalama yameandikwa. Kwa hii Katiba ya sasa you cannot read anything about majeshi lakini yameandikwa kwa Katiba and ana attempt to control them. halafu kuna what we called wakati wa civic education, imagined constitutional issues. Mambo ya walemavu yameandikwa hapo na mambo ya mazingira yameandikwa hayo na mambo kama hayo. Ukilinganisha Katiba ya zamani those things were not there that is why we call them imagined constitutional issues. Hiyo ni kwa ufupi lakini mengine mengi nyinyi mtaangalia. Pengine hamjasoma sana hii Katiba lakini kwanza tunasema kwa Kiingereza yule anvaa viatu anajua mahali inafinya so even without reading you should know na kuisoma hii ingawa watu wetu wamecomplain kwamba ni lugha ya lawyers. Hii sio lugha ya lawyer hii. ukilinganisha na hii, hii ni lugha ile inatakiwa lawyer asome na kukueleza vile inasema. Tumejaribu sana kuandika kwa lugha ya kueleweka na tumetafsiri kwa kiswahili. Hii Katiba iko kwa lugha ya lawyers na ya kiingereza pekee yake ingawa kama sisi Watume tulikuwa na pocket Verson ambayo tulikuwa tunatumia kwa civic education. Asante.

Caroline: Ngoja kwanza. Asante sana bwana Mosonik. Saa hii tungependa tupate reactions from your new people. Mtupatie maswali halafu tutajaribu kujibu. Sasa ningetaka tukuwe na order kidogo. Ukitaka kuuliza maswali weka mikono juu halafu utajibiwa. -----inaudible.

Philip Mitei: Jina langi ni Philip Mitei. Swali yangu tumesika sasa hakutakuwa na Provincial Administration. Assistant chief watakuwa under Provincial, watakuwa nje ama wapi? Maswali zingine nimesikia tunaanzia chini na macouncillors. Sikusikia mnataja macouncillors. Watachaguliwa wapi? Asante.

Caroline: Majibu mtapatiwa baadaye.

Grace Maina: *Kongoi missing en ng'alek tugul che kagemwa che ba iman. Ng'alek tugul che ka ng'alal bichu ko ng'alek ab iman*

Translator: Haya yote yameelezwa na hawa wote ni ya ukweli.

Grace: *Ko amun kaba iman ii,*

Translator: Kwa sababu ilikuwa ya ukweli sana

Grace: *Ko kamwae ale kagas tebutyet en yonon ne ba MPs,*

Translator: Kuna swali ambalo ningetaka kuuliza kuhusu kiti cha Ubunge

Grace: *Kounoton ko MP ko to tinye uwezo ko ng'alal en bunge,*

Translator: Anauliza ya kwamba member ya Bunge anaweza kuuliza maswali huko Bunge. Huenda nauliza hivyo kwa sababu inasemekana kama kiti kile kingine ya uwaziri ambayo ataletwa kutoka nje ya Bunge ambao hatachaguliwa

Grace: *Ana member puch?*

Translator: Ama atakuwa tu mtu wa kawaida?

Grace: *kounoton awekyini kongoi en baisionik che karoyai,*

Translator: Kwa hivyo tunawarudishia asante sana kwa kazi yeyote ambaye mmewai kufanya.

Grace: *Ko malelen amwa chechang', kainenyun ko Grace Maina.*

Translator: Kwa majina anitwa Grace Maina asante sana

Grace: *Aba yuton.*

Translator: Yeye ni mkaaji wa Kiptere.

Joseph Tere: Mimi naitwa Joseph Tere na ningetaka niulize kwamba ni Provinces ngapi ambao walipendelea majimbo? Swali ni hiyo tu.

Chende Sang: My name is Chende Sang. My question is you talk of government will provide basic needs like water, shelter, medical services. Suppose the government does not provide these services to a citizen, what must a citizen do?

Geoffrey Samoei: Yangu ni kufuatana na vile imeandikwa kwa karatasi. Jina ni Geoffrey Samoei. Kwanza ni katika ile chapter one ninaye kwa ile mbili ama kwa tatu ambayo inasema supremacy of the constitution an enforcement of the constitution. Ninapendekeza hiyo iwe ni kitu ambayo itapendekeza. Na kitu ionginge iwe ni mbili, saba na katika ile chapter mbili, saba na kumi na kumi na tatu. Hiyo inasema katika chapter ya saba, territory labda tuseme direct rally, ile Province yetu mali zote isiende katika Central Government. Iwe ndani ya Province na katika saba, nane, capital, Province isiwe Nairobi. Itolewe Province kwa mambo ya kuminimize fedha zetu. Yaani iwe Province sawa kama kawaida. Hata mambo

ya constituencies itolewe.

Chapter tatu, sijui nitakuwa nimemaliza.....niendele. Kwa chapter ya tatu kwa mambo ya

(End of tape two side A) and values and principles. Hii national goals kitu ambacho mtu mwingine alikuwa anauliza ni kwamba serikali asipotufanyia kitu tutafanya namna gani? Tuangalie labda kama President asipotufanyia ambao tunafanya hata yeye atolewe halafu tuchague mwingine. Kwa maana pengine mtu anaweza kuja kutuambia kitu ambao haendi kufanya huko. Itolewe.

Chapter ya nne ambayo ni sehemu ishirini na saba ambao inasema powers of Parliament... powers of Parliament inachagua Commissioners zote halafu ikichagua ma Commissioners kama ni Secretaries itakuwa ni sisi ndiyo tumechagua hawa Commissioners. Kwa sababu kutakuwa na mtu mwingine ambaye anaenda kuchagua Commissioners, nini mambo yote itakuwa , hatukuchagua hawa Commissioner of Police, Commissioner ya mashamba, itoke kwa Parliament. Isitoke kwa namna ingine halafu hiyo imeturusisha hata na sisi.

Chapter ya tano ambayo inasema nitazungumzia thelathini na mbili, arobaine na nne, na arobaine na nne na hamsini na tatu, sitini na saba, sitini na sita, sitini na tano, na sitini na saba na sitini na tisa. Thelathini na mbili inasema right to live. Mtu akiuliwa labda mtu mwingine anaweza kuuwa mwingine. Itakuwa inamkataza kuishi kama mwanadamu mwenzie. Sasa ikifungwa maisha haitakuwa mzuri. Ama mtu akitoa maisha ya mtu auliwe hata yeye pia. Itoke tu evidence kwamba aliuwa mtu. Na tukiwacha namna hiyo sasa mtu atasema hafadhali mimi nifungwe milele lakini nitoe maisha ya huyu. Kwa hivyo hiyo right to live haitakuwa mzuri mtu akienda kufungwa milele, na baadaye asemehe.

Arobaine na nne inasema freedom of religion, belief and opinion. Freedom of religion na kanisa. Unajua saa zingine hii kanisa sijui mambo yake sana kwa maana ni dini. Tunaye makanisa mingi ya kikristo, ya kislamu hata Waindi watakuja hapa Kenya, watuhubirie na tutaingia hiyo. Makanisa hata ya kabila yetu sio kama ile ya Mungiki. Hapana. Lakini ya ukabila kwa vile hata saa hii wakalenjin iko na kanisa yetu. Ndiyo ninasema kwamba kikitokea labda siku ingine tupate makanisa mabao wazee walijua ya kikwetu, sio mbaya. Serikali amepatia sisi lakini iwe registered tupate kanisa mzuri ya kinyumbani.

Kitu kingine 48, mimi naangalia kufanya haraka haraka. Freedom of association, mambo ya kufanya mkutano isiwe inatolewa peana permission kutoka kwa polis ama mahali pengine. Kitu mzuri Assistant Chief ametolewa lakini polis. Hiyo freedom ya association isitokee sisi ya kufunga hiyo maneno kwa maana isipokuwa tu manmeno machafu isitokee huko lakini watu wakutane wapate freedom.

Hamsini na tatu ambayo inasema freedom of trade and occupation and profession. Hii biashara iendele hata zaidi. Iendele kawaida vile tulikuwa tunafanya kwa maana restriction isipokuwa tu labda wewe ndiyo ukataliwe ununuliwe kutoka sehemu

ambayo unaenda ni shauri yako lakini biashara iendelee kwa Kenya nzima namana hiyo ndiyo maana hata mimi naunga mikono.

Sitini na tano, nataka nifanye haraka haraka kwa maana hata watu wengine wanataka pia kuongea. Fair Administration, yaani hutumwa mzuri ambayo hata nasi tunataka kwa maana hatutaki mambo ambao saa ingine inafanywa namana hii, mimi nafikiria hawa watu wengi wanafikiria namna hii. Vile tulikuwa tuko katika ile sheria ya huku nyuma ya utumwa ya ile nyuma lakini saa hii tunataka fair administration. Hii ni kusema kwamba hata hii Commission ya kutunga sheria isitolewe ili tuendelee kufanya nini kutoa maoni kwa maana hii ni muda kidogo sana na mtuasitirestrict kwamba Commission isimame. Hii sio administration mzuri. Nani huyo sasa anatoa sheria namna hiyo. Tunataka watu wa Kenya wamesema Commission iendelee iendelee mpaka wamalize kazi hata elections fine. Tusifanyiwe haraka haraka namna hiyo.

69 ambayo inasema ya kwamba fair trial, hiyo ni kwa kortini. Hii mambo ya ma advocates ambao wanaenda kusumbua watu huku na huku kuwafanyia watu biashara ambao saa ingine hata inasiumbukiza mtu ambao hakuwa na makosa ndani ya jela hatutaki. Tunataka fair trial mzuri. Haya katika ile chapter ya sita nitaenda kwa sehemu ya sabini ya saba ambao inasema ya kwamba elections zifanywe na kuhesabiwa hapo hapo na vitu vyote iwe fast katika Commission ya kufanya mambo ya elections ili kusitokee mambo kama zile za zamani. Ifanywe kwa hapo na ihesabiwe kwa hapo na iwe fast ili hii mambo ya kupelekwa na gari isiwe.

Sehemu ingine ni ile chapter ya nane sehemu ya mia moja na sita na mia moja na saba. Nitaunga tu mkono hapo nikisema members of National Council and members of National Assembly. Isipokuwa ningependekeza kwamba, hii member of National Council, iwe katika district halafu hata sheria kidogo kidogo ziwe zinatoka kwa district level halafu inakuwa na maasiliano yaani ile relation ya national. Iwekwe hii macoucillor itoke kwa district na apeleke sheria halafu hiyo inarelate na ile kwa maan sheria hatuakuwa tukitengeneza leo na tumalize leo. Kwa mfano; kama sisi Wakalenjin tunataka sheria kama nikikamatwa nisiwe na makosa niende nifanyiwe nihukumiwe huko kortini kwa sheria za mila zetu. Kitu kama hiyo tu. Nihukumiwe kwa sheria za kinyumbani ndiyo maana mimi nasema kwamba hiyo Council Assembly ya district iwe inatengeneza kitu kama hiyo.

Chapter ya nane ndiyo nitazungumzia mia moja hamsini na nne, mia moja hamsini na tatu na mia moja sabini na moja na sabini na saba. Hapa ndiyo inasema kwamba, 164 inasema kwamba retainment of Presidential power. President asikuwako na nguvu kama vile ilikuwako zamani. Akiiba kitu ndani, akifanya kitu ambao landa saa ingine haja vunja hii sheria yetu hii awekwe ndani kwa maana aafe kwamba nitachunga ile Katiba ya wananchi na akienda kuvunja huku awekwe ndani. Asivutwe tu kwa maana atakuwa ametudharau.

163 inasema kwamba impeachment and removal of the President naunga mkono tena hapo. 171, nipeleke haraka haraka. Appointment of Prime Minister iwe ya Parliament sio President ndiyo inaapoint Prime Minister. Parliament ndani kama

wale Commissioner halfu President asikatumie kwa mambo ya kivyake. Tunataka Prime Minister atoke ndani yha Parliament, kura kutoka kwa Parliament halafu Prime Minister aeshimu Parliament. Sio aheshimu mtu mmoja. Aheshimu Parliament.

Kitu ingine ambao ni 77 inasema ya kwamba assignment of functions. Kazi ya Prime Minister mimi nafikiria isiwe ni mtu ya nje tu kutuombea sisi mambo ya pesa huko nje na mambo zingine. Asiingie mambo ya ndani ya hapa nyumbani. Iwe tu akitekeleza mambo yake ya huko nje.

Haya katika chapter ya sita sasa kwa sehemu ya mia moja tisaini na nne nina mambo kutoka hapo inasema kwamba appointment of judges. Appointment of judges iingie tena ndani ya Parliament. Hawa hawana chama ya Bunge ambao watasema kwamba tumechoka. Waende wa appoint judges kutokana na qualifications yao. Mtu ambaye amehudumu kwa muda mrefu na ambaye records yake ni mzuri awe ana appoint ndani ya Parliament na lawyers wapeane makaratasi yao kwa Parliament. Watu wa Bunge wanangalia wanasema huyho anakuwa wa kweli anakuwa mzuri bila partiality yoyote. Hiyo inafanywa namna hiyo.

Haya kitu kingine mimi karibu nimalize kwa sababu nimechukua muda mrefu sana. Chapter ten sehemu ya 220 inasema ya kwamba, powers of district government, civil servants zote. waalimu, askari, madaktari iwe inalipwa kutokana na resources ya district isiwe tena ikitokea kitu kama strike ya teachers. Mishahara yote inaangaliliwa kutoka wapi? Kwa district halafu pesa zote itoke huko kwa central government, iingie kwa district halafu district inadistribute anangalia vile mishahara yao iko. Halafu mwalimu ambayo ataona kwamba haikutosheleka na hiyo mishahara aende. Akiangalia kwamba anatosheka na hiyo mishahara aendelee na kazi. Kwa maana saa ingine tukiweka zote kwa kitabu moja sisi wananchi tutaumia kwa mambo ya strike kila siku.

Kitu kingine ni chapter 14, 260 powers and functions of the Public Service Commission. Parmanet Secretaries wote ni Public Service Commission, wote iwe watoe hizo powers katika Commissioner ambao pia Commissioner inachaguliwa na Parliament halafu isinyanyase watu.

266 appointment of Police Commissioner, nilikuwa nimemaliza hapo kwamba anachaguliwa kwa Parliament.

Kitu kingine 18, 294 ni constitution amendment. Hii constitution amendment ni nyinyi kama Commission. Muendeleo halafu labda siku ingine tutakuja kubadilisha kitu ingine tena kwa hizi ambao labda hatujui ama kuongeza. Hiyo Commission iendelee kufanya kazi kwa district mpaka wapi, National. Asante.

Joseph Kiptum Arap Koech: Asante sana jina langu naitwa Joseph Kiptum Arap Koech. Yangu nitatoa maoni moja tu kwa sababu mimi naona kitu ambayo inashinda sisi kwa hii mambo ya constitution ambayo insumbia sisi hawa watu wote na kama sisi tunakubaliana kitu kimoja kwa dunia hii ni tofauti. Hiyo ni kitu ambayo inafanya sisitunakuwa tofauti kwa njia

zote ambao tunataka. Sasa haja yangu ni kusema kuliko kuwa na hii chama mingi na hakuna kitu ambao wanatengeneza kwa maoni yangu binafsi vile nimeona hizi political parties. Tukiwa na political parties tatu tu peke yake kwa maoni yangu ile iko kwa serikali na ile ina oppose naingine ya tatu ni kuchunga hawa halafu wanaweka namna hiyo. Hiyo kazi itaendelea vizuri. Sasa itafanya sisi wote tukubaliane kitu moja na tukifanya tutafaulu.

Ingingine mimi naenda kwa mambo hii ya religious kwa sababu kwa maoni yangu sioni sababu gani tuweni chama hata hii ya religious ingawa nikisema ni ya makanisa lakini kwa maoni yangu ni kama political party tu. Haja gani kuwe na kanisa saba na mimi najua Mungu moja tu, Biblia ni moja. Hapana tatu. Ukiona kanisa mbili tu peke yake kwa maoni yangu. Ya Jumapili na ya Jumamosi. Wale ambao wanapumzika Jumamosi wafanye kazi jumapili kwa sababu Mungu ni moja. Tukubaliane. Hiyo sasa tutakosa hii mambo ya mimi nataka kuwa mkubwa upande hi nataka kuwa mkubwa pande hii. Hiyo ndiyo inaumiza sisi na tukiomba kitu kimoja safari moja Mungu haikatai anasikia na utafaulu. Hata tukitaka kutawala kama wenzangu tukubaliana kitu kimoja Mungu atakuja hapa kwetu kutu tendea sisi kitu chochote. Tukienda kitu kimoja. Hapana zungumza maneno mingi na mimi.

Ingingine kwa maoni yangu hii ya mashamba mimi naona hakuna haja mimi nikiwa na plot karibu eka kumi na niko na watoto saba. Sasa kila mtoto kama atakuwa miaka kumi na nane atataka shamba lakini ukiona haja yake tu ni kuenda kuuza hilo shamba. kesho akichukua anaenda kuuza. Mimi maoni yangu naona shida ya vijana ikiwa kwa society ama kwa community kama village ya clan. Hizi shamba ziwe owned by clans na ni hawa clans wenyewe wataamua itakuwa namna gani. Na hiyo tutapatia watoto wetu kazi. Hakuna kazi ingine kwenda kutafuta kwa shamba huko mashambani. Kazi iko nyumbani. Tukiwapatia watoto wetu na tuwaambie wewe lima hapa leo, wewe panda maharagwe, huyu panda viazi, huyu apande cabbage pesa itakuja. Hakuna haja ya kuenda kutafuta kazi pahali pengine. So this should be owned by the land.

Ingingine ni hii mambo ya marriage. Kwa maoni yangu tuko na marriage ya serikali na tuko na ya kanisa na hii ya kienyeji ya nyumbani vile vile tuweke sheria kwwa sababu kuna wengine hii ya nyumbani, mtoto wako akitaka msichana ameona msichana ya fulani yuko mzuri anachukua anaoa kwa wa kisiri huko. Haambii mimi. Kesho anasema anataka kumfukuza anaita wazee wa kijiji ati mimi nimekataa na hii mwanamke anataka kumfukuza. Na wakati wa kuoana hakumwambia kitu. Walikuwa wanaibana. Sasa hii mamboya kuibana ajabu sheria iwekwe kwa wazee. Mtu akitaka kuoana kwanza alete wazee aseme kwa nini anataka kuwa bibi wa pili. Sijakataa bibi kuolewa hata kama ni kumi lakini *ogigilgei ko yon mache kebarait komakichabe oret kobarait kotiech chito kobarait ak konde kwondo oloton. Nyalu konde kwando oloton kosir konyokoyamo tugul en yu. Makichilegei ngwany yache atokosta au.*

Translator: Huyu mzee ameeleza ya kwamba kabla hujaoa bibi wa pili au wa tatu ama wa kiasi fulani, bado umetengeneza mahali penye hawa wote watakaa. Sio tu kuo. Tena ikiwa hata ni ya kimila lazima ujulishe wazee wengine wajue ili watoe idini yao kama huyo mtu mwenye wanataka kuoana ni watu halali ama hapana.

Ingingine mimi natoa ni hii haki hii ya kifo kama mtu ameuwa mwingine. Mimi kwa maoni yangu sioni kwa sababu gani anasema anafungwa maisha. Hata kufanywa hiyo maisha mimi naona nikua tu ni kukufa tu kwa sababu siweji ona yeye tena. Ajambo yeye auliwe saa hii halafu wale wengine wanaona wakose kusema kuenda kusifu kama wewe unaua mtu hata wewe unawawa lakini ikiambiwa utafungwa maisha kuna wengine wanaweza fikiria njia ingine lakini kufungwa maisha hii anaenda kutafuta njia ingine. mara -----(inaudible) kesho unasikia ametolewa ameenda Tanzania amenda Uganda. Anataka kurudi na watu wake na huko ameumiza watu wote.

